**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**(TAMISEMI)**
**MANISPAA YA MOROGORO**
**SHULE YA SEKONDARI KILAKALA**

Telegramu: **"MKUU WA SHULE KILAKALA"**
**Simu Mkuu wa Shule: 0713907755**
**Simu Shule: 0710 417541**
FAX No. 023-260 0407
Tafadhali unapojibu taja:
E-mail: kilakalass1957@gmail.com
Tovuti: www.kilakalasps.ac.tz

**Shule ya Sekondari Kilakala**,
S. L .P 40,
**MOROGORO**

Kumb. Na......................................

Tarehe: 15/04/2025

**PICHA**
***(awe na shati jeupe)***

Mwanafunzi ........................................................................

**YAH: - MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO**
**SHULE YA SEKONDARI KILAKALA MWAKA 2025**

**a)** ***Karibu Shuleni Kilakala.***

Kwa niaba ya kamati ya uchaguzi, ninayo furaha kukuarifu rasmi kwamba umechaguliwa kujiunga na shule hii **KIDATO CHA TANO** mwaka 2025 kwa mchepuo wa: **HGL, CBG, PCB, PCM**, **PMCs.** "**DAIMA MBELE NYUMA MWIKO**" Maneno haya ndiyo **KAULI MBIU YA SHULE (MOTO)** au mwongozo wa shule yetu. Kama umeridhia kujiunga na shule hii, huna budi kuitafakari kauli hiyo na kuichukulia kwa uzito unaostahili.

Shule ya Sekondari ya Wasichana Kilakala, ipo umbali wa kilometa tano tu kutoka Kituo Kikuu cha mabasi ya Morogoro kinachoitwa **Msamvu na** km 14 kutoka katika stesheni ya **Jakaya Kikwete (kituo cha SGR)**. Usafiri kutoka kituoni hapo kuja shuleni unapatikana. Nauli kwa taxi ni kati ya **shilingi 10,000/=** hadi shilingi **15,000/=** na kutoka SGR mpaka Shuleni nauli kwa bajaji ni kati ya Tshs **12,000/=** hadi **15,000/=** na Taxi ni kati ya **15,000/=** na **20,000/=.** Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe **8/07/2025**

**MUHIMU: -** Endapo utachelewa zaidi ya **wiki mbili tangu tarehe ya kutangazwa kuripoti shuleni utakuwa umepoteza nafasi hii. Taarifa za Shule zitatolewa na mkuu wa Shule kwa namba 0713907755, na makamu Mkuu wa Shule 0718406363**

**NB:Kilakala sekondari ni shule ya vipaji maalumu kitaaluma, mwanafunzi atadhihirisha kuwa na kipaji hicho kwa kufaulu katika masomo yake yote.**

**b)** ***Mambo muhimu ya kuzingatia:-***

***2.1*** **Sare ya shule:-**

**a) Sare ya darasani (zinapatikana kwa fundi namba hii 0715-018537 ili kuepuka utofauti wa mshono na rangi za sketi.)**

- Sketi mbili rangi ya ***Dark blue*** (Marinda ya box, na ndefu iguse kiatu).

- ❖ Mashati mawili meupe aina ya tomato, mikono mifupi, yenye "collar" na mfuko kwa kila shati.
- ❖ Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba, vyenye visigino vifupi (muundo kama viatu vya kiume). **Buti haziruhusiwi.**
- ❖ Soksi nyeupe jozi nne (au Zaidi) zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi.
- ❖ Sweta moja rangi ya *Dark blue***.**
- ❖ Kwa watakaovaa **hijabu**, waje na mashati **mawili** meupe ya **mikono mirefu** (aina Tomato), **Majuba** yanayofunika mikono rangi nyeupe (**mawili**).

**b) Sare ya kazi:- (zinapatikana kwa fundi namba hii 0715-018537 ili kuepuka utofauti wa mshono na rangi za sketi.)**

- ❖ Sketi mbili rangi ya dark blue (Marinda ya box, na ndefu iguse kiatu)**.**
- ❖ T - shirt tatu round rangi ya njano**. (Ziwe nzito zisioneshe ndani)**
- ❖ Kwa watakaovaa hijab, yanayofunika mikono za rangi ya njano mbili**.**

**c) Sare za michezo:-** Raba nyeusi, track suit rangi bluu bahari (light blue). Wakati wa michezo kila mwanafunzi atalazimika kuvaa sare ya michezo hivyo **aje nazo.**

**d)** Wanafunzi watavaa sare ya darasani **wakati wa vipindi** na sare ya kazi **baada ya muda wa vipindi**.Nguo za nyumbani **HAZIRUHUSIWI KABISA**, hivyo **asije nazo**.

**e)** Aje na blanketi moja kwa ajili ya baridi, shuka nne; (02 rangi ya pinki na 02 rangi ya blue bahari).

**f)** Aje na mto wa kulalia mmoja wenye foronya nne (04) 02 za rangi ya pinki na 02 za rangi ya bluu bahari.

**g)** Aje na sanduku la chuma moja linalotosha vitu vyote. **(Mabegi hayaruhusiwi)**

**TANIBIHI:** Kuanzia ukurasa wa 11 unaonesha mavazi ya mwanafunzi shuleni. **Tafadhali** zingatia mavazi hayo kwani mwanafunzi hatapokelewa ikiwa mavazi yake yatakuwa tofauti.
Muhimu:-

***2.2 Aje na shangazi kaja kubwa kwa ajili ya kuwekea madaftari na vitabu darasani pamoja na* Ream mbili (02) za karatasi za photocopy kwa kila muhula.**

***2.3 Michango mingine ya shule:-***

i) Michango mingine ni:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Mchango ya uendeshaji wa Shule | - shilingi | 65,000/= |
| ii. | Tahadhari | - shilingi | 5,000/= |
| iii. | Nembo | - shilingi | 5,000/= |
| iv. | Kitambulisho cha Shule | - shilingi | 5,000/= |
| | | | **Jumla - TSH, 80,000/=** |

**MUHIMU: -** Ulipaji wa ada na michango yote ufanyike tawi lolote la **Benki ya NMB.** ***Jina la akaunti ni: -*** **Headmistress, Kilakala Secondary School**. **Namba ya Akaunti 22101100070**.
Fedha ilipwe **kabla ya kufungua shule**. Tafadhali wasiliana na karani wa benki ili **aandike jina la mwanafunzi na kidato chake**. Risiti ya Benki (pay in slip) utakuja nayo **siku ya kufungua shule**. Toa photocopy**, leta nakala halisi** (original copy) baki na kivuli kwa **ajili ya kumbukumbu**. **HATUPOKEI FEDHA TASLIMU HIVYO USIJE NAZO**

**TANIBIHI:**

i. Umfungulie mwanao akaunti katika benki ya NMB au CRDB, shuleni aje na kadi yake. Fedha zote za matumizi yake shuleni, mzazi/ mlezi ingiza katika akaunti yake.

**h) *Orodha ya vitu ambavyo mwanafunzi anavyotakiwa kuleta:-***

a) Madaftari makubwa ya kutosha kulingana na masomo yake. Kuanzia kumi na moja (11) na kuendelea (Counter books quire 4).

b) Nguo za ndani za kutosha (chupi za kike, vesti za kike, “underskirts"/shimizi,sidiria) na za kulalia ( night dress za suruali za kike).
c) Njoo na godoro futi mbili na nusu(2.5) godoro zuri lisiloumiza mgongo na liwe na kava ya ngozi.**(Shuleni hakuna magodoro)**
d) Vyombo vya kulia chakula (kontena lenye mfuniko, kikombe na kijiko).
e) Ndoo mbili (02).
f) Kitenge (jozi moja tu)
g) Chandarua cheupe kimoja (01) cha pembe nne.
h) Taulo, mswaki na dawa ya meno, sabuni na mafuta ya kupaka.
i) Koti la mvua au mwamvuli.
j) ***Vifaa vya usafi: -***
    - Toilet/scrubing brush (01),
    - Hard broom (fagio la brashi ngumu 01),
    - Rubber squeezer (fagio la kusukumia maji 01),
    - Sabuni za maji nzito za kusafishia choo lita tano **(EMINA au LIT),**
k) Vitabu vya ibada kwa mujibu wa dhehebu/dini yako.
l) Koti jeupe kwa ajili ya maabara (Laboratory coat) kwa wanaochukua masomo ya Sayansi tu; yaani (Physics, Chemistry na Biology).
m) "**Dissecting kit yenye nta (wax)**" na "**Dissecting try**" kwa wanaosoma **Biology** tu.
n) Shule ina nakala za vitabu kwa ajili ya masomo utakayochukua; hata hivyo kama unaweza kupata vya kwako binafsi uje navyo. ( list ya vitabu imeambataniswa uk 10 - 11 )
o) Kwa wanafunzi wa michepuo ifuatayo (**PCM, PMCs**, **PCB na CBG**) kila mmoja aje na **STOP WATCH YA KUVAA SHINGONI NA NI LAZIMA**" kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo na "**SCIENTIFIC CALCULATOR FUNCTION 991**".
p) Leta result slip ya Kidato cha Nne **muhimu**.
q) Leta nakala ya cheti cha kuzaliwa **muhimu**.
r) Kama una **Bima ya afya** njoo nayo, kama huna mzazi au mlezi **mkatie binti yako Bima ya Afya.**

**i) *Afya ya mwanafunzi:-***

Mara upatapo barua hii mwone **Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali** iliyo karibu nawe, ili upimwe kuthibitisha kuwa una afya ya kutosha kusoma masomo ya sekondari. Fomu maalum imeambatanishwa na barua hii. Mara utakapofika shuleni ioneshe ikiwa imejazwa na kugongwa muhuri katika Hospitali za serikali tu. Shule haitoi chakula maalum (special diet) kwa wagonjwa. Hata hivyo ni:-

**Ni marufuku kuja na chakula cha aina yoyote hapa shuleni. KAMA MWANAFUNZI ANA CHANGAMOTO YA AFYA, TAFADHALI TOA TAARIFA KWA MKUU WA SHULE NA KUKABIDHI TAARIFA YA MAANDISHI KUTOKA KATIKA HOSPITALI YA SERIKALI.**

**j) *Sheria za shule:-***

a) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote .
b) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wanafunzi wenzake, kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, jiko la shule n.k.
c) Yakupasa kuweka shule, eneo lake na wewe binafsi katika hali ya usafi wakati wote.
d) Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa.
e) Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani na wakati wa kujisomea.
f) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua, ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na **Mkuu wa Shule.**
g) **Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, "earphones" pamoja na redio**.
h) Mwanafunzi haruhusiwi **kupiga simu popote** bila kibali cha uongozi wa shule. Mawasiliano yote yatafanywa kupitia **ofisi ya Mkuu wa Shule, Makamu Mkuu wa Shule, Wataaluma wa Shule na Matroni wa Shule.**
i) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja, au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani.

j) Mwanafunzi haruhusiwi **kufanya mazungumzo** na ndugu/jamaa yake msikitini, kanisani, au hospitalini. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane na **uongozi wa shule**.

k) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika **nyumba za walimu** au **wafanyakazi wengine** bila ruhusa maalum.

l) **Mafuta yenye harufu kali, Mafuta yanayobadilisha ngozi ya mwanafunzi (kujichubua), perfume/spray, poda, rangi za kucha na midomo, wanja, curl, nywele za bandia, mapambo kama bangili hereni, mikufu n.k. havitakiwi kabisa shuleni. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na kucha ndefu wala kujipamba.**

m) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, wimbo wa shule, wimbo wa Tanzania Tanzania Nakupenda kwa Moyo Wote na Tazama Ramani, (Kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizi)

n) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi, (Mwanafunzi mgonjwa anapaswa kupumzika katika zahanati ya shule).

o) Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na **nywele fupi wakati wote** wawapo shuleni, urefu **unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana**. Hairuhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama kiduku, kijoti, kiseven n.k.

p) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo hapa shuleni.

q) Ni marufuku **kumruhusu mgeni** kufika katika **eneo la mabwenini**.

r) Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu ambaye si mwanajumuiya wa shule hii isipokuwa **kwa kumsalimia**.

s) Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anaruhusiwa **kumwombea ruhusa mwanafunzi** kama kuna tatizo. Pia ndiye **atakayekuja shuleni** pindi atakapohitajika kufanya hivyo.

t) Wakati wa kufunga shule wanafunzi wote wataondoka **kwa pamoja kwa usafiri utakaoratibiwa na shule**. Hakuna **ruhusa yoyote itakayotolewa mapema** kabla ya **siku rasmi ya kufunga shule**.

u) Kama mwanafunzi atapatikana na kosa la nidhamu, mzazi au mlezi ndiye atakayetakiwa kufika shuleni na si mtu mwingine yeyote kama babu, bibi, mjomba,shangazi, kaka n.k.

v) Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule. Hivyo mwanafunzi:-
   i. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
   ii. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
   iii. Ahudhurie kwenye kazi atakayopangiwa
   iv. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call), ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba, mikutano ya darasa na maabara za shule.
   v. Ahudhurie vipindi vyote vya dini.
   vi. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.

w) **NI LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali (pass) cha maandishi.

**MUHIMU:**

❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.**

❖ **Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu**

❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**k)** ***Mwanafunzi atafukuzwa shule au kusimamishwa masomo iwapo atapatikana na kosa kati ya haya yafuatayo*:-**

a. Kutukana/kutumia lugha chafu, kumpiga mwalimu au mwanafunzi mwenzake
b. Kupigana na mwanafunzi mwenzake.
c. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine.
d. Kuolewa.
e. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya uongozi wa shule na utoro wa muda mrefu (miezi 03).
f. Biashara, ulevi na kutumia dawa za kulevya.
g. Kuwa na mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
h. Kuingia na kushiriki kwenye vilabu vya pombe na nyumba za kulala wageni au nyumba zinazouza pombe (Guest house au Bar)
i. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
j. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani.
k. Wizi.
l. Kudharau bendera ya Taifa.
m. Makosa ya jinai.
n. Kunyanyapaa wengine.
o. Kuleta **simu ya mkononi** au **kukutwa na viambatanishi vyak**e kama charger, betri, vocha, line n.k.
p. Uasherati, ubakaji, na usagaji.
q. Kutokuhudhuria vipindi darasani na au kutokufanya mitihani na majaribio kwa makusudi.
r. Kukaa au kulala bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi nje.
s. Kutohudhuria vipindi vya dini

Kama unakubaliana na **haya yote** yaliyoelekezwa na **uko tayari kuyatii** na **kuyatekeleza**; tia saini katika fomu iliyoambatanishwa. Fomu hii ya kujiunga na shule inatakiwa **irudishwe ofisini** pamoja na **fomu ya kupimwa iliyojazwa na mganga** wa hospitali **ya serikali**.

Nakutakia safari njema.

**KARIBU SANA**

MARY D. LUGINA

**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
KILAKALA SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 40, MOROGORO

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………………………………………………………………………

Nimesoma na kuelewa yote yaliyoelekezwa kwenye barua ya kujiunga na shule.
Ninaahidi kuwa nitajifunza kwa bidii zangu zote, nitazingatia sheria za shule kama zilivyoainishwa, nitazifuata na nitakuwa na nidhamu wakati wote kwa manufaa yangu, ya shule na ya Taifa kwa jumla.
**Kwa kuzingatia yote niliyo soma katika maelekezo,** Pia endapo nitakiuka taratibu na kanuni za shule nitakuwa tayari kurudi nyumbani kumuita mzazi/mlezi wangu ………………………………………………………………… (Jina la mzazi/mlezi) au kusimamishwa masomo.

…………………………………………… ………………………….
**Jina na sahini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

**AHADI YA MZAZI**

Mimi…………………………………………Mzazi/mlezi wa ………………………………. ninaahidi kushirikiana na shule wakati wote kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata maelekezo yote na kutekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa.

……………………………………………… ……………………………….
**Saini ya Mzazi / Mlezi** **Tarehe**

**………………………………………**
**Namba ya simu**

KILAKALA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 40,
**MOROGORO.**

DATE .............

Ref. No...............................................

**PART A:-**
To the Medical Officer,
.........................................................
.........................................................
**REF: .........................................................................................................................**
Please examine the above-named student as to her physical and mental fitness for being student. Each defect will hinder a girl for Secondary Schools' education.

1. a). Eye sight..............................................................................
   b). Hearing...............................................................................
   c). Limbs...................................................................................
   d). Speech.................................................................................
   e). Venereal disease..................................................................
   f). Leprosy...............................................................................
   g). Epilepsy..............................................................................

2. Neurosis...........................................................................................
3. Other serious diseases........................................................................
4. Pregnancy.........................................................................................

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a **GOVERNMENT MEDICAL OFFICER**)
I have examined the above-named student and confirm that she is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a). | Eye sight .................................... | f). | Leprosy.............................. |
| b). | Hearing .......................................... | g). | Epilepsy............................... |
| c). | Limbs ............................................. | h). | Neurosis........................... |
| d). | Speech ............................................ | i). | Other serious diseases........... |
| e). | Venereal diseases ........................... | j). | Pregnancy....................... |

Name..........................................................Signature........................... Date...........................

**STATION**............................................................ **DESINATION**..................................................
**N.B.,** I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.

**FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1.JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………………………

2. JINA LA MZAZI WA MWANAFUNZI………………………………………………

3. KAZI YA MZAZI WA MWANAFUNZI……………………………………………

4.JINA LA SHULE ANAKOTOKA…………………………………………………………………

5.TAREHE YA KUZALIWA……………………………………………………………………………

6.KATA ANAYOTOKA MWANAFUNZI……………………………………………………………

7.WILAYA ANAYOTOKA MWANAFUNZI………………………………………………………

8.MKOA ANAOTOKA MWANAFUNZI………………………………………………………………

9.KABILA…………………………………………………………………………………………………

10.URAIA………………………………………………………………………………………

11.DINI/DHEHEBU……………………………………………………………………………………

12. ANUANI YA MZAZI……………………………………………………………………

13. NAMBA YA SIMU YA MZAZI - NYUMBANI…………………………………………………
- OFISINI……………………………………………………………………
E - MAIL ADRESS………………………………………………………………………………

14. MAJINA MANNE YA NDUGU WA KARIBU WALIOIDHINISHWA KUCHUKUA NAFASI YA MZAZI/MLEZI ENDAPO DHARURA ITATOKEA: -

| Na | JINA | UHUSIANO | ANAKOISHI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 01. | | | | |
| 02. | | | | |
| 03. | | | | |
| 04. | | | | |

**KILAKALA SECONDARY SCHOOL**
**A-LEVEL BOOKS REQUIREMENT**

**GEOGRAPH PAPER I**

1. Principles of Physical Geography- by F.J Monkhouse
2. A comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School- by D.T Msabila
3. Practical Geography for Africa by John M. Prichard
4. Land forms in Africa – An introduction to Geomorphology – by Colin Buckle
5. Africa – by J.M. Prichard
6. Practical Geography for A level – by Francis Mnyawi
7. Practical Geography for A level – by TIE
8. Physical Geography for A level – by TIE

**GEOGRAPH PAPER II**

1. Human and Economic Geography – by Goh cheng & Morgan
2. Advanced Level geography Course book –by Tanzania Institute of Education ( TIE)
3. An Integrated Focal regional study on Human and Economic Geography Advanced level paper 2- by D.T Msabila

**ENGLISH LANGUAGE I**

1. English for Advanced Secondary School student's book Form V- by TIE
2. English language for Advanced learners edition 2014 by N. Ashley

**ENGLISH LANGUAGE II**

**A. NOVELS AND SHORT STORIES**

i) Chinua Achebe – A man of the people
ii) Ayi Ewei Armah – The Beautiful ones are not yet born
iii) Soga – His Excellence the head of state.

**B. PLAYS**

i. I will marry when I want by Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii
ii. An Enemy of the people by H. Ibsen
iii. Betray in the city by F. Imbuga

**C. POETRY**

i. Tanzania Institute of Education – Selected poems
ii. The wonderful Surgeon – by C. Mloka

NB: Make sure you come with TWO tiltles from each part.

This list of English Language is meant for HGL students only.

**HISTORY**

i. Rodney, W – How European Underdeveloped Africa
ii. Lenin V.I. Imperialism the highest stage of capitalism
iii. World Map, Africa Map, East Africa Map and Tanzania Map.
iv. World History (I & II) by Idrissa Ramadhan Msuya
v. History for Advanced secondary school by TIE

**PHYSICS**

1. PRINCIPLES OF PHYSICS CLASS XI ,By S. Chand's
2. PRINCIPLES OF PHYSICS CLASS XII ,By S. Chand's
3. PHYSICS FORM V By TIE
4. PHYSICS FORM VI By TIE

**MATHEMATICS**

1. Pure mathematics Vol. 1 by
2. Pure mathematics Vol. 2
3. Engineering Mathematics
4. Statistics for A- level
5. Understanding Mathematics.
6. Advanced mathematics for secondary school (I &II) by TIE

**CHEMISTRY**

1. New Understanding Chemistry for Advanced Level Third Edition (2000). By Ted Lister, and Janet Renshaw
2. Essentials of Physical Chemistry 28th Edition (2022). By Bahl Arun, Bahl B.S. & Tuli G.D.
3. Conceptual Chemistry volume I by S.K.JAIN & Dr. Shailesh K. JAIN. 6th edition (2006).
4. Conceptual Chemistry volume II by S.K. JAIN & Dr. Shailesh K. JAIN. Reprinted (2017).

**BIOLOGY**

1. Taylor D., Green N & Stout G. Biological Science : 3rd edition 1&2
2. Robert M.B. New Biology a Functional approach 4th edition
3. Glenn and Susan. New understanding Biology 4th edition
4. S.O.Loeje – Certificate Practical Biology
5. C.Advanced Biology- Principles and Applications

**COMPUTER SCIENCE**

1. Computer science for Advanced Secondary School form V by TIE
2. Computer science for Advanced Secondary School form VI by TIE
3. Website Development and Ethics

Note: Knowledge is Acquired through Books but Skills is Obtained by Practice.
Bring with you at least two books from list above

**MFANO WA SARE ZA SHULE ZINAZOTAKIWA**




Juba kwa waislamu


sare za michezo


sare kamili pamoja na sweta


Tshirt ya njano


juba la kazi